**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA SITA

# YATOKANAYO NA KIKAO CHA NANE

**08 FEBRUARI, 2017**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA NANE**
**TAREHE 8 FEBRUARI 2017**

## I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Mhe. Andrew John Chenge (Mwenyekiti) alisoma Dua na kuongoza Kikao.

**Makatibu Mezani:**

1 Ndg. Theonest Ruhulabake
2 Ndg. Lawrence Makigi
3 Ndg. Neema Msangi

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

1 Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

2 Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

## III. MASWALI:

### 1 OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na. 81: Mhe. Khamis Mtumwa Ali [Kny Mhe. Abbas Ali Mwinyi].

Swali Na. 82: Mhe. Ruth Hiyob Mollel

Nyongeza:

i. Mhe. Ruth Hiyob Mollel
ii. Mhe. Kasuku Samson Bilago

### 2 OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Swali Na. 83: Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare

Nyongeza: Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare

### 3 WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Swali Na. 84: Mhe. Abdallah Dadi Chikota

Nyongeza:
i. Mhe. abdallah Dadi Chikota
ii. Mhe. Cecil David Mwambe
iii. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate

Swali Na. 85 : Mhe Hasna Sudi Katunda Mwilima

Nyongeza: Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima

**4 WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Swali Na. 86: Mhe. Rashid Mohammed Chuachua

Nyongeza:

i. Mhe. Rashid Mohammed Chuachua
ii. Mhe. Sebastian Simon Kapufi

Swali Na. 87: Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo

Nyongeza:

i. Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo
ii. Mhe. Vedestus Mathayo Manyinyi
iii. Mhe. Joseph Roman Selasini
iv. Mhe. Venance Methusalah Mwamoto

**5 WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Swali Na. 88: Mhe. Vedasto Edgar Ngombale

Nyongeza:

i. Mhe. Vedasto Edgar Ngombale
ii. Mhe. Riziki Shahari Mngwali
iii. Mhe. Kabwe Zuberi Zitto

**6 WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Swali Na. 89: Mhe. Mary Pius Chatanda

Nyongeza:

i. Mhe. Mary Pius Chatanda
ii. Mhe. Martha Jachi Umbulla
iii. Mhe. Rhoda Edward Kunchela

Swali Na. 90: Mhe. Zaynab Matitu Vullu

Nyongeza:

i. Mhe. Zaynab Matitu Vullu
ii. Mhe. Margareth Semwanza Sitta

7 **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**
Swali Na. 91: Mhe. Asha Abdullah Juma

Nyongeza:

i. Mhe. Asha Abdullah Juma
ii. Mhe. Maryam Salum Msabaha

8 **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Swali Na. 92: Mhe. Asyharose Ndogholi Matembe

Nyongeza:

i. Mhe. Asyharose Ndogholi Matembe
ii. Mhe. Hassan Seleman Kaunje
iii. Mhe. Jesca David Kishoa

9 **WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Swali Na. 93: Mhe. Faida Mohammed Bakari (Kny Mhe. Maida Hamad Abdallah)

Nyongeza:

i. Mhe. Faida Mohammed Bakar
ii. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako

## IV. MATANGAZO:

1 Wageni waliokuwepo Bungeni walitambulishwa na Kiti akiwemo Balozi Tuvako Manonga.

2 Vikao vya Kamati mbalimbali vilitangazwa pamoja na Matangazo mengine.

## MWONGOZO WA SPIKA:

1. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa aliomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) na 46 kuonyesha kutoridhika na majibu ya Swali Na. 88 kuhusu nani aliongoza Vita ya Majimaji. Kwani wanafunzi hufundishwa ni Kinjekitile. Aliomba mwongozo Serikali itoe kauli ni nani? Kama siyo Kinjekitile historia itakuwaje? Fidia italipwaje?

   Mwenyekiti alijibu kwamba, kutokana na majibu ya Serikali kupitia nchi za Afrika Mashariki watafikisha suala hilo ili kuona kama fidia italipwa. Ikiwa

Kinjekitile ndiye aliyeongoza Vita hiyo au wengine itabdi historia iandikwe upya. Alisisitiza kusubiri majibu ya Serikali.

2. Mhe. Abdallah Ally Mtolea aliomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) na 46(1) kuhusu kujibu Swali Na. 90 kwamba, anaona Serikali haionyeshi kuguswa na suala la Watoto wa kike kupata ujauzito kwa kusema mpaka ikutane na wadau na kwamba yeye haoni sababu kwani Wabunge ni wadau wa watoto wa kike na pia alihitaji kujua kama Swali hilo alitendewa haki.

   Mwenyekiti alijibu Mwongozo huo kwamba, kwa kuwa Serikali imesema ipo sheria ambayo imetungwa na Bunge, hivyo kama kuna tatizo katika sheria iletwe ipitiwe na kurekebishwa. Mwenyekiti aliagiza Serikali ijipange haraka kuleta marekebisho hayo.

3. Mhe. Joseph Osmund Mbiliyi aliomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7) kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika Jiji la Mbeya ambalo halina maji kabisa. Alisema ipo hatari ya kipindupindu kwa ugonjwa huo. Na pia alitoa ushauri wa namna ya kupata maji kuokoa Jiji la Mbeya kwani hali ni mbaya.

   Mwenyekiti alijibu kwamba, kwa kuwa suala hilo halijaja kwa kuzingatia Kanuni kwani si jambo lililotokea mapema Bungeni. Hivyo atumie Kanuni inayohusika kuweza kuleta hoja yake ili Serikali wafanyie kazi.

4. Mhe. Mwikwabe Mwita Waitara alisimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), 50 na 51 kuomba mwongozo kuhusu maelezo binafsi akitaka kuleta, alete wakati gani? Sasa au baadae?

   Mwenyekiti alimuelekeza Mhe. Mwita Waitara kusoma Kanuni ya 50 kuona mpangilio wa hoja Binafsi jinsi inavyoelekezwa. Kasha amwandikie Spika kueleza nia yake na yale yatakayoelezwa katika hoja hiyo wakati utakapofika na Spika akimruhusu atapewa muda wa kuwasilisha Bungeni.

5. Mhe. Hasunga Haonga alisimama kwa Kanuni ya 68(7) kuhusu mtu mmoja aitwaye Saanane ambaye amepotea na hajulikani alipo. Kwa kuwa Faru John alipotea na fedha nyingi ilitumika kumtafuta; nani anathamani zaidi kati ya mtu na huyo Faru?

   Mwenyekiti alimjibu kwamba, Kanuni ya 68(7) inahusu jambo lililotokea mapema Bungeni, habari ya Faru John siyo jambo lililotokea mapema Bungeni wala Bunge halimtambui huyo Saanane. Hivyo Mbunge alete suala hilo kwa utaratibu mwingine.

6. Mhe. John Wegesa Heche aliomba Mwongozo na kutoa ombi kuhusu kusudio la kuleta Maelezo Binafsi ya Mbunge, hivyo alipewa nafasi hiyo kusema nia yake.

Hoja yake ilihusu kukamatwa kwa Wabunge bila *notification* yoyote hata katika Majimbo yao, jambo linalofanywa na DC's (Wakuu wa Wilaya) jambo linaloshusha heshima ya Bunge.

Mwenyekiti alimshauri Mhe. John W. Heche kuliwasilisha jambo hilo katika Kamati ya Haki na Madaraka ya Bunge ili kutoa nafasi ya Bunge kujadiliana na Serikali kutafuta mwafaka.

## V. HOJA ZA SERIKALI:

Hoja ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma.

Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuchangia hoja za Kamati hizo kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu – Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira;

2. Mhe. Albert Obama Ntabaliba – Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

3. Mhe. Juma Selemani Nkamia - CCM

4. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia - CCM

5. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo - CCM

## VI. KUSITISHA BUNGE:

Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni.

## VII. BUNGE KURUDIA:

Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia na Hoja ya Kamati za Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ziliendelea kuchangiwa kama ifuatavyo:-

### MWONGOZO WA SPIKA:

1. Mhe. Abdallah Hamis Ulenga aliomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68 (7) kwa jambo lilitokea leo kuhusu kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam (Mhe. Paul Makonda) kuonyesha dalili ya kulidhalilisha Bunge, kwamba "Wabunge hawana jipya bali kulala Bungeni". Mhe. Abdallah Ulenga aliendelea kusema kuwa, kwa kauli hiyo Mhe. Paul Makonda yafanyike moja kati ya mambo matatu:-

a) Waziri Mkuu achukue hatua za makusudi ili kulinda heshima ya Bunge.

b) Kwa kutumia Kanuni za Bunge, Hoja hii ipelekwe kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

c) Mhe. Paul Makonda aombe radhi kupitia vyombo vya habari.

2. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa aliomba Bunge litumie Kanuni ya 51 na 52 kujadili Hoja hiyo ya udhalilishaji wa Bunge kwa kauli iliyotolewa na Mhe. Paul Makonda (Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam) ili hadhi ya Wabunge iweze kulindwa.

**UAMUZI WA MWENYEKITI:**

Mwenyekiti alizuia Hoja hiyo isijadiliwe kwa kuwa bado jambo hilo ni la kusikia na yeye mwenyewe hajamsikia Mhe. Paul Makonda, hivyo ni vyema suala hilo lipelekwe katika Kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ili kuthibitika kama kweli Mhe. Paul Makonda alisema hayo na wapi na kama ni suala linaloingilia Haki na Madaraka ya Bunge.

Pia, Mwenyekiti alisisitiza kwamba, iwapo Mtanzania yeyote ameathirika na matamshi ya Wabunge, wanayo haki ya kuandika kwa Spika na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itashughulikia suala hilo.

Mwisho aliwaelekeza Wabunge kwamba, nao wakiona wameathirika kwa namna yoyote na matamshi hayo, wanayohaki ya kuleta malalamiko yao kwa Spika na kushughulikiwa katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Uchangiaji wa Taarifa za Kamati uliendelea kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | Mhe. Anatropia Theonest Lwehikila | - | CHADEMA |
| 7. | Mhe. Joseph Leonard Haule | - | CHADEMA |
| 8. | Mhe. Abdallah Hamis Ulenga | - | CCM |
| 9. | Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete | - | CCM |
| 10. | Mhe. Leonidas Tutubert Gama | - | CCM |
| 11. | Mhe. Omary Tebweta Mgumba | - | CCM |
| 12. | Mhe. Hawa Subira Mwaifunga | - | CHADEMA |
| 13. | Mhe. Riziki Said Lulida | - | CUF |
| 14. | Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma | - | CCM |
| 15. | Mhe. Daniel Nswanzugwako | - | CCM |
| 16. | Mhe. Dkt. Deodorus Buberwa Kamala | - | CCM |
| 17. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya | - | CCM |
| 18. | Mhe. Zainab Athumani Katimba | - | CCM |
| 19. | Mhe. Cecil David Mwambe | - | CHADEMA |
| 20. | Mhe. Esther Nicholas Matiko | - | CHADEMA |
| 21. | Mhe. Khatib Said Haji | - | CUF |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 22. | Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu | - | CCM |
| 23. | Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka | - | CCM |
| 24. | Mhe. Mwanne Ismael Mchemba | - | CCM |

**MATANGAZO:**

Wageni waliokuwepo Bungeni walitambulishwa na Kiti.

Uchangiaji kwa upande wa Serikali uliendelea kama ifuatavyo:-

25. Mhe. Joelson Luhaga Mpina
26. Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango
27. Mhe. George Mcheche Masaju
28. Mhe. Januari Yussuf Makamba
29. Mhe. Prof. Sospter Mwijarubi Muhongo
30. Mhe. Charles John Mwijage

Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu - Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, alihitimisha Hoja yake, alitoa Hoja na baada ya kuungwa mkono Bunge lilihojiwa na kupitisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati hiyo.

Mhe. Albert Obama Ntabaliba - Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma alihitimisha Hoja yake, alitoa Hoja na baada ya kuungwa mkono Bunge lilihojiwa na kupitisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati hiyo.

## VIII. HOJA YA KUVUNJWA KWA HAKI ZA BUNGE:

Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara alitoa Maelezo ya Hoja yake kuhusu kuvunjwa kwa Haki za Bunge kufuatia Kitendo cha Mkuu wa Wilaya ya Arumeru (Mhe. Anthony Pastory Mnyeti) kuandika maneno yanayodhalilisha Bunge. Hoja ya Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara iliungwa mkono na kuchangiwa na Wabunge wafuatao:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. John Peter Kadutu | - | CCM |
| 2. | Mhe. Ester Amos Bulaya | - | CHADEMA |
| 3. | Mhe. Kabwe Zitto Zuberi | - | ACT |
| 4. | Mhe. Saed Ahmed Kubenea | - | CHADEMA |
| 5. | Mhe. Msukuma Joseph Kasheku | - | CCM |
| 6. | Mhe. George Mcheche Masaju | - | Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 7. | Mhe. Jenista Joakim Mhagama | - | Waziri wa Nchi (OWM) |

Baada ya mjadala, Mtoa Hoja Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara aliotoa Mapendekezo yafuatayo ambayo yalipitishwa kuwa Maazimio ya Bunge:-

(a) Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Alexander Pastory Mnyeti na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul Makonda waitwe kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili wajieleze na itakapothibitika kuwa wamevunja Sheria na kudhalilisha Bunge basi wachukuliwe hatua za kinidhamu;

(b) Mamlaka za kinidhamu ziwawajibishe ikiwa ni pamoja na kuachia nafasi hizi kwa sababu wameshindwa kuzitumia vizuri;

(c) Waziri mwenye dhamana atoe maelekezo mahsusi kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya juu ya namna ya kufanya kazi zao bila kuingilia Mihimili mingine na hasa kudhalilisha Wabunge katika maeneo yao ya kazi;

(d) Vyombo na mamlaka nyingine zinapokuwa zinafanya kazi na zikihitaji Wabunge kwa mashitaka ya aina yoyote ile itakuwa ni muhimu au ni lazima Spika wa Bunge ajulishwe.

## IX. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 2.15 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi Tarehe 9 Februari, 2017 Saa 3.00 Asubuhi.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **08 FEBRUARI, 2016** | **KATIBU WA BUNGE** |